
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

TAARIFA YA TAKWIMU ZA VYAMA VYA USHIRIKA

JULAI 2025 – JUNI 2026



JULAI, 2026

YALIYOMO

MUHTASARI WA TAARIFA iii
ORODHA YA MAJEDWALI iv
ORODHA YA MAUMBO v
VIFUPISHO vi
SURA YA KWANZA 1
Utangulizi 1
SURA YA PILI 2
Idadi ya Vyama vya Ushirika 2
Vyama vya Ushirika Vilivyofutwa 2025/2026 3
Vyama vya Ushirika vya wanawake 5
SURA YA TATU 7
Takwimu za wanachama wa Vyama vya Ushirika 7
SURA YA NNE 9
Makusanyo na Mauzo ya mazao Kupitia Vyama vya Ushirika pamoja na Usambazaji wa Pembejeo 9
Uchambuzi wa Taarifa ya Mali za Kudumu za Vyama vya Ushirika 12
Uchambuzi kwa Aina ya Mali 12
(a) Majengo 12
(b) Mashamba 12
(c) Mashine na Mitambo 13
(d) Viwanda 13
(e) Viwanja 13
(f) Vyombo vya Moto 13
(g) Maghala 13
(h) Mifumo ya TEHAMA 13
Uchambuzi wa Ushiriki wa Vyama kwenye Mfumo wa MUVU 13
Mali za Ushirika kwa ujumla zimeongezeka thamani sokoni. 13
SURA YA TANO 14
Ajira zilizotolewa kupitia vyama vya ushirika 14
SURA YA SITA 15
6.1MUHTASARI WA UTENDAJI 15
6.2HALI YA UTENDAJI WA SACCOS KWA MWAKA 2024 NA 2025 18
Hitimisho 19

MUHTASARI WA TAARIFA

Taarifa hii inatoa muhtasari wa takwimu za Sekta ya Ushirika kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Juni 2026, Taarifa imetokana na uchambuzi wa takwimu za Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU).

Lengo ni kutoa picha kamili ya hali ya usajili wa vyama, wanachama, mauzo ya mazao, mali na ajira zinazotokana na Sekta ya Ushirika.

Kwa ufupi

i. Hadi kufikia Juni 2026, jumla ya Vyama vya Ushirika 6,577 vimesajiliwa kwenye MUVU, na Vyama 577 vimefutwa kwa mwaka 2025/2026 kutokana na vyama hivyo kuwa sinzia.

ii. Jumla ya Wanachama 3,667,635 wamesajiliwa kwenye Vyama vya Ushirika, kati yao Wanaume ni 2,341,512 (63.8%) na Wanawake ni 1,326,123 (36.2%).

iii. Jumla ya Kilo 1,699,390,580 za mazao mbalimbali ziliuzwa kwa mwaka 2025/2026 zenye thamani ya TZS 4,283,691,725,392, ikilinganishwa na Kilo 1,834,085,262 zenye thamani ya TZS 3,024,616,683,786 kwa Mwaka 2024/2025.

iv. Vyama vya Ushirika vimetoa Ajira 161,279 ikilinganishwa na Ajira 154,966 zilizotolewa kuishia Juni 2025, ikiwa ni ongezeko la Ajira 6,313.

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1:Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa kwenye MUVU kufikia Juni 2026 2

Jedwali 2: Idadi ya Vyama vilivyofutwa kwa Mwaka 2025/26 3

Jedwali 3:Idadi ya vyama vya Ushirika vya wanawake 6

Jedwali 4:Wanachama wa Vyama vya Ushirika waliosajiliwa kwenye MUVU 7

Jedwali 5: Makusanyo na mauzo ya mazao kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26 9

Jedwali 6: Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo kupitia Ushirika.....10

Jedwali 7:Mali zinazomilikiwa na Vyama zilizosajiliwa kwenye MUVU 11

Jedwali 8: Ajira zilizotolewa na Vyama vya Ushirika 14

Jedwali 9: Viashiria vya Utendaji wa SACCOS.....15

ORODHA YA MAUMBO

Umbo 1: Idadi ya vyama vilivyosajiliwa kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26 3

Umbo 1: Mikoa yenye idadi kubwa ya Vyama.....5

Umbo 3: Mikoa yenye idadi ndogo ya Vyama.....5

Umbo 4: Idadi ya vyama vya Ushirika vya Wanawake..... 6

Umbo 5: Mgawanyo wa Wanachama kwa Jinsia..... 8

Umbo 6: Idadi ya Wanachama kwa Umri na Jinsia 8

Umbo 7: Kiasi cha Mazao (Kilo) kilichouzwa kwa mwaka 2024/25 na 2025/26 9

Umbo 8: Mazao yaliyouzwa kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26 kupitia Ushirika.....10

Umbo 9: Idadi ya Mali zinazomilikiwa na Vyama 12

VIFUPISHO

i. TCDC – Tanzania Cooperative Development Commission
ii. SACCOS – Savings and Credit Cooperative Society
iii. AMCOS – Agricultural Marketing Cooperative Society
iv. MUVU – Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika

SURA YA KWANZA

Utangulizi

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ni Taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Sura ya 211 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2025. Majukumu ya msingi ya Tume ni Kusimamia, Kudhibiti na Kuhamasisha maendeleo ya vyama vya ushirika nchini.

Malengo ya Taarifa ya Takwimu

i. Kutoa takwimu sahihi na za kina kuhusu vyama vya ushirika; na

ii. Kufuatilia mwenendo wa ukuaji wa sekta ya ushirika.

Wigo wa Taarifa

Taarifa ya Takwimu inatoa Muhtasari kitwakimu wa utekelezaji na mwenendo wa maendeleo ya sekta ya ushirika nchini Tanzania kwa kipindi cha Julai, 2025 – Juni, 2026, katika maeneo yafuatayo:

i. Usajili wa Vyama na Wanachama wa vyama vya ushirika kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU);

ii. Idadi ya Vyama vilivyofutwa;

iii. Idadi ya Wanachama wa Vyama Vya Ushirika;

iv. Makusanyo na Mauzo ya mazao kupitia Vyama vya Ushirika;

v. Usambazaji wa pembejeo za Kilimo kupitia Ushirika;

vi. Mali zinazomilikiwa na Vyama vya Ushirika; na

vii. Ajira zinazotolewa na Vyama vya Ushirika.

Chanzo cha Takwimu

Takwimu zilizotumika katika Taarifa hii zimetokana na uchambuzi wa takwimu kutoka kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) na vyanzo vingine vya Tume.


SURA YA PILI

Idadi ya Vyama vya Ushirika

Hadi kufikia Juni 2026, Idadi ya Vyama vilivyosajiliwa katika Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ilikuwa **6,577** ikilinganisha na kipindi kilichopita ambapo idadi ya Vyama ilikuwa ni **6249**. Mchanganuo wa vyama hivyo kimkoa ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1

Jedwali 1:Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa kwenye MUVU kufikia Juni 2026

Na	MKOA	Aina za Vyama vya Ushirika								Juni, 2025		Juni, 2026	
		SACCOS		AMCOS		Vyama Vikuu na Miradi ya pamoja	Vyama vinginevyo		Awali	Jumla Kuu		Jumla Kuu	
		Jumla	Asilimia	Jumla	Asilimia	Jumla	Jumla	Asilimia	Jumla	Jumla	Asilimia	Jumla	Asilimia
1	ARUSHA	123	1.9	53	0.8	1	15	0.2	2	189	3.0	194	2.9
2	DAR ES SALAAM	275	4.2	1	0.0	3	45	0.7	0	310	5.0	324	4.9
3	DODOMA	57	0.9	36	0.5	3	25	0.4	1	116	1.9	122	1.9
4	GEITA	25	0.4	254	3.9	3	30	0.5	0	298	4.8	312	4.7
5	IRINGA	39	0.6	70	1.1	5	19	0.3	1	139	2.2	134	2.0
6	KAGERA	37	0.6	334	5.1	2	10	0.2	5	378	6.0	388	5.9
7	KATAVI	3	0.0	43	0.7	1	7	0.1	2	52	0.8	56	0.9
8	KIGOMA	10	0.2	167	2.5	2	27	0.4	3	201	3.2	209	3.2
9	KILIMANJARO	76	1.2	96	1.5	13	18	0.3	0	208	3.3	203	3.1
10	LINDI	11	0.2	176	2.7	2	7	0.1	0	191	3.1	196	3.0
11	MANYARA	34	0.5	49	0.7	1	17	0.3	0	99	1.6	101	1.5
12	MARA	30	0.5	215	3.3	2	35	0.5	9	286	4.6	291	4.4
13	MBEYA	85	1.3	206	3.1	6	63	1.0	4	368	5.9	364	5.5
14	MOROGORO	50	0.8	161	2.4	7	44	0.7	1	240	3.8	263	4.0
15	MTWARA	9	0.1	403	6.1	3	9	0.1	16	435	7.0	440	6.7
16	MWANZA	30	0.5	214	3.3	1	33	0.5	0	277	4.4	278	4.2
17	NJOMBE	48	0.7	68	1.0	3	30	0.5	10	166	2.7	159	2.4
18	PWANI	34	0.5	96	1.5	1	17	0.3	1	141	2.3	149	2.3
19	RUKWA	11	0.2	74	1.1	1	5	0.1	0	71	1.1	91	1.4
20	RUVUMA	15	0.2	223	3.4	3	15	0.2	1	246	3.9	257	3.9
21	SHINYANGA	16	0.2	228	3.5	4	14	0.2	60	300	4.8	322	4.9
22	SIMIYU	4	0.1	316	4.8	1	1	0.0	27	348	5.6	349	5.3
23	SINGIDA	12	0.2	105	1.6	2	19	0.3	12	134	2.1	150	2.3
24	SONGWE	12	0.2	187	2.8	1	21	0.3	31	234	3.7	252	3.8
25	TABORA	14	0.2	438	6.7	3	17	0.3	301	637	10.2	773	11.8
26	TANGA	51	0.8	83	1.3	4	62	0.9	0	185	3.0	200	3.0
	JUMLA	**1111**	**16.9**	**4296**	**65.3**	**78**	**605**	**9.2**	**487**	**6249**	**100**	**6577**	**100**



Umbo 1: Idadi ya vyama vilivyosajiliwa kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26


2.2 Vyama vya Ushirika Vilivyofutwa 2025/2026

Jedwali 2: Idadi ya Vyama vilivyofutwa kwa Mwaka 2025/26


Na.	Mkoa	Vyama vya Kifedha	Vyama visivyo vya Kifedha	Jumla
1	ARUSHA	20	4	24
2	DAR ES SALAAM	67	10	77
3	DODOMA	14	5	19
4	GEITA	8	18	26
5	IRINGA	12		12
6	KAGERA	9	4	13
7	KATAVI	2	3	5
8	KIGOMA	12		12
9	KILIMANJARO	16	27	43
10	LINDI	1	1	2
11	MANYARA	18	8	26
12	MARA	7	4	11
13	MBEYA	9	14	23
14	MOROGORO	21	3	24
15	MTWARA	1		1
16	MWANZA	13	10	23
17	NJOMBE	19	13	32

Na.	Mkoa	Vyama vya Kifedha	Vyama visivyo vya Kifedha	Jumla
18	PWANI	8	15	23
19	RUKWA	12	49	61
20	RUVUMA	9	4	13
21	SINGIDA	9	2	11
22	SONGWE	3	29	32
23	TABORA	3	31	34
24	TANGA	23	7	30
	TOTAL	**316**	**261**	**577**

Mikoa yenye Idadi kubwa ya Vyama na Mikoa yenye idadi ndogo ya vyama



Umbo 2: Mikoa yenye idadi kubwa ya Vyama




Umbo 3: Mikoa 5 Yenye idadi ndogo ya Vyama

Vyama vya Ushirika vya wanawake

Idadi ya Vyama vya Ushirika vya Wanawake

Jedwali 3:Idadi ya vyama vya Ushirika vya wanawake

Na.	MKOA	SACCOS	AMCOS	UVUVI	MAZIWA	MWANI
1	ARUSHA	4	0	0	0	0
2	DAR ES SALAAM	3	0	0	0	0
3	DODOMA	1	1	0	0	0
4	GEITA	1	0	0	0	0
5	IRINGA		2	0	0	0
6	KAGERA	1	0	0	0	0
7	KILIMANJARO	0	1	0	4	0
8	MANYARA	2	0	0	0	0
9	MOROGORO	1	0	0	0	0
10	MWANZA	2	0	1	0	0
11	PWANI	1	0	0	0	1
12	RUKWA	0	2	0	0	0
13	SINGIDA	0	1	0	0	0
	JUMLA	**16**	**7**	**1**	**4**	**1**




Umbo 4: Idadi ya vyama vya Ushirika vya Wanawake

SURA YA TATU


Takwimu za wanachama wa Vyama vya Ushirika

Jedwali 4:Wanachama wa Vyama vya Ushirika waliosajiliwa kwenye MUVU

Na.	Mkoa	Wanaume	Wanawake	Jumla
1	ARUSHA	19,195	16,336	**35,531**
2	DAR ES SALAAM	155,928	141,790	**297,718**
3	DODOMA	12,313	10,853	**23,166**
4	GEITA	48,965	15,691	**64,656**
5	IRINGA	15,731	6,762	**22,493**
6	KAGERA	76,819	47,310	**124,129**
7	KATAVI	37,558	11,639	**49,197**
8	KIGOMA	25,272	7,207	**32,479**
9	KILIMANJARO	91,325	64,020	**155,345**
10	LINDI	269,388	254,870	**524,258**
11	MANYARA	10,317	3,771	**14,088**
12	MARA	25,585	9,138	**34,723**
13	MBEYA	57,851	27,676	**85,527**
14	MOROGORO	31,898	36,047	**67,945**
15	MTWARA	326,745	163,126	**489,871**
16	MWANZA	96,160	22,164	**118,324**
17	NJOMBE	17,018	14,348	**31,366**
18	PWANI	72,826	33,809	**106,635**
19	RUKWA	41,015	22,457	**63,472**
20	RUVUMA	103,878	84,241	**188,119**
21	SHINYANGA	111,724	69,819	**181,543**
22	SIMIYU	475,659	148,925	**624,584**
23	SINGIDA	21,597	9,584	**31,181**
24	SONGWE	80,539	14,625	**95,164**
25	TABORA	100,962	76,352	**177,314**
26	TANGA	15,244	13,563	**28,807**
	JUMLA KUU	**2,341,512**	**1,326,123**	**3,667,635**



Umbo 5: Mgawanyo wa Wanachama kwa Jinsia




Umbo 6: Idadi ya Wanachama kwa Umri na Jinsia

SURA YA NNE


Makusanyo na mauzo ya mazao kupitia Vyama vya Ushirika pamoja na usambazaji wa Pembejeo

Jedwali 5: Makusanyo na mauzo ya mazao kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26

Na	MAZAO	2024/2025		2025/2026		ASILIMIA YA UFANISI (%)	
		UZITO (KILO)	MAUZO (SHILINGI)	UZITO (KILO)	MAUZO (SHILINGI)	UZITO	THAMANI
1	TUMBAKU	2,506,398	672,639,747,631	177,855,573.47	1,160,640,652,860.70	98.6	42.1
2	KAHAWA	32,628,620	182,935,286,474	71,916,628	939,806,494,704	54.6	80.5
3	PAMBA	61,870,627	93,112,191,722	215,672,157	257,437,114,583	71.3	63.8
4	KOROSHO	219,182,495	838,785,555,277	439,688,000	1,302,671,446,650	50.2	35.6
5	UFUTA	145,297,428	534,429,302,261	192,051,545	484,973,254,908	24.3	-10.2
6	KAKAO	5,936,297	133,143,444,592	1,581,176	7,448,453,256	-275.4	-1,687.50
7	SOYA	1,204,200	1,812,093,471	1,057,952	5,751,342,240	-13.8	68.5
8	MBAAZI	94,242,650	187,794,042,622	35,577,357	34,118,685,363	-164.9	-450.4
9	DENGU	18,473,781	36,535,780,841	4,165,857	4,974,033,258	-343.5	-634.5
10	MKONGE	61,215,555	238,740,645,000	6,743.91	21,551,338,695	-907,616	-1,007.80
11	CHAI	24,825,000	9,085,950	14,640	54,581,698	-169,470	83.4
12	CHOROKO	2,220,301	3,097,319,895	8,583,510	13,268,332,421	74.1	76.7
13	MIWA	1,159,237,910	98,013,413,050	551,203,040	50,930,394,755	-110.3	-92.5
14	MAHINDI	5,241,000	3,557,675,000	0	0	-	-
15	PARETO	3,000	11,100,000	16,400	65,600,000	81.7	83.1
JUMLA KUU		**1,834,085,262**	**3,024,616,683,786**	**1,699,390,580**	**4,283,691,725,392**	**-7.93**	**29.39**



Umbo 7: Kiasi cha Mazao (Kilo) kilichouzwa kwa mwaka 2024/25 na 2025/26



Umbo 8: Thamani ya Mazao yaliyouzwa kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26 kupitia Ushirika


Jedwali 6: Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo kupitia Ushirika

AINA YA PEMBEJEO	*2024/2025*		*2025/2026*		ASILIMIA YA UFANISI	
	IDADI	THAMANI (SHILINGI)	IDADI	THAMANI (SHILINGI)	**IDADI**	**THAMANI**
MBOLEA (TANI)	2,134,459	282,031,846,652	2,138,621	259,209,454,588	0.19	-8.80
VIUATILIFU VYA UNGA (TANI)	62,538	165,597,024,280	35,123.680	91,802,151,500	-78.05	-80.38
VIUATILIFU VYA MAJI (LITA)	4,446,652	120,077,294,236	4,717,688	230,147,575,850	5.75	47.83
VIFUNGASHIO - MAGUNIA (PCS)	6,206,788	49,599,046,355	7,189,209	52,102,497,550	13.67	4.80
MBEGU (TANI)	647,022	822,035,800	82,111	224,101,500	-687.98	-266.81
Jumla	**13,497,459**	**618,127,247,323**	**14,162,753**	**633,485,780,988**	**4.70**	**2.42**

TAARIFA YA MALI ZA KUDUMU ZA VYAMA VYA USHIRIKA KUISHIA TAREHE 31 DECEMBER, 2025

Jedwali 7: Mali zinazomilikiwa na Vyama zilizosajiliwa kwenye MUVU

NA	AINA YA MALI	IDADI YA MALI	THAMANI YA AWALI (SHILINGI)	THAMANI YA SOKO (SHILINGI))
1	Majengo	1,448	704,726,848,339	825,938,572,211
2	Mashamba	416	65,398,214,002	272,334,862,992
3	Mashine na Mitambo	620	32,059,161,580	22,168,222,010
4	Viwanda	242	33,901,804,800	35,824,874,225
5	Viwanja	756	79,193,681,733	129,982,689,025
6	Vyombo vya Moto	557	44,617,065,085	14,988,085,432
7	Maghala	849	45,951,240,991	58,008,676,282
8	Mifumo ya Tehama	102	-	980,688,268
JUMLA KUU		4,990	1,005,848,016,530	1,360,226,670,445
A	IDADI YA VYAMA VYA MSINGI VILIVYOINGIZA MALI KWENYE MFUMO WA MUVU			3,639
B	IDADI YA VYAMA VYA UPILI VILIVYOINGIZA MALI KWENYE MFUMO WA MUVU			70
	JUMLA KUU			**3,709**



Umbo 9: Mali za Kudumu za Vyama vya Ushirika

4.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Mali za Kudumu za Vyama vya Ushirika

Muhtasari wa Jumla

i. Jumla ya mali: 4,990
ii. Thamani ya awali: Shilingi 1,005,848,016,530
iii. Thamani ya soko: Shilingi 1,360,226,670,445
iv. Ongezeko la thamani: Shilingi 354,378,653,915 (ongezeko la takriban 35%)

Hii inaonesha kuwa kwa ujumla mali za Vyama vya Ushirika zimeongezeka thamani sokoni, jambo linaloashiria uimara wa uwekezaji wa muda mrefu.

4.2 Uchambuzi kwa Aina ya Mali

(a) Majengo

i. Idadi: 1,448 (idadi kubwa zaidi)
ii. Thamani ya soko imeongezeka kwa takriban Shilingi bilioni 121 (~17%)
iii. Ni msingi mkubwa wa mtaji wa kudumu.

(b) Mashamba

i. Ongezeko kubwa sana la thamani (kutoka Shilingi bilioni 65 hadi bilioni 272)
ii. Ukuaji wa zaidi ya 300%
iii. Inaashiria kupanda kwa thamani ya ardhi na uwekezaji wa kilimo.

(c) Mashine na Mitambo

i. Thamani imeshuka kutoka Shilingi bilioni 32 hadi Shilingi bilioni 22 (~-31%)
ii. Inaonesha uchakavu (depreciation) au teknolojia kupitwa na wakati.

(d) Viwanda

i. Ongezeko dogo (6%)
ii. Inaashiria uwekezaji wa viwanda unaendelea kuwa thabiti.

(e) Viwanja

i. Ongezeko la takriban 64%
ii. Thamani ya ardhi mijini inaendelea kupanda.

(f) Vyombo vya Moto

i. Kushuka kwa zaidi ya 66%
ii. Inaonesha uchakavu mkubwa au matumizi makubwa.

(g) Maghala

i. Ongezeko la takriban 26%
ii. Inaonesha kuimarika kwa miundombinu ya uhifadhi.

(h) Mifumo ya TEHAMA

i. Thamani ya soko Shilingi milioni 980
ii. Hakukuwa na thamani ya awali (inaweza kuwa mali mpya)
iii. Inaashiria mwelekeo wa kidigitali.

Uchambuzi wa Ushiriki wa Vyama kwenye Mfumo wa MUVU

i. Vyama vya Msingi: 3,639
ii. Vyama vya Upili: 70
iii. Jumla: 3,709

Hii inaonesha ushiriki mkubwa wa vyama vya msingi katika kuingiza taarifa za mali, lakini vyama vya upili vina mchango mdogo kwa idadi.

i. Mali za Ushirika kwa ujumla zimeongezeka thamani sokoni.
ii. Ardhi (mashamba na viwanja) ndiyo mali iliyoongeza thamani zaidi.
iii. Mali zinazochakaa kama vyombo vya moto na mashine zimepungua thamani.
iv. Kuna dalili ya kuimarika kwa uwekezaji wa miundombinu na TEHAMA.
v. Mfumo wa MUVU umetumiwa zaidi na vyama vya msingi kuliko vya upili.

SURA YA TANO

Ajira zilizotolewa kupitia vyama vya ushirika

Hadi kufikia Juni 2026, jumla ya Ajira zilizotolewa kupitia Vyama vya Ushirika ni 161,279 ikilinganisha na 154,966 katika kipindi cha Juni 2025 ikiwa ni ongezeko la ajira 6,313.

Kati ya ajira zilizotolewa, ajira 116,707 (72.39%) ni ajira za mkataba zinazotokana na Miradi inayoendeshwa na Vyama vya Ushirika 44,572 (27.61%) ni ajira za kudumu.

Jedwali 8: Ajira zilizotolewa na Vyama vya Ushirika

NA	Mkoa	Waajiriwa	Mikataba	Jumla
1	ARUSHA	1,066	867	1,933
2	DAR ES SALAAM	4,081	297	4,378
3	DODOMA	659	78	737
4	GEITA	3,471	20,679	24,150
5	IRINGA	919	180	1,099
6	KAGERA	3,465	32,145	35,610
7	KATAVI	728	757	1,485
8	KIGOMA	899	911	1,810
9	KILIMANJARO	2,690	511	3,201
10	LINDI	4,914	6,587	11,501
11	MANYARA	227	236	463
12	MARA	465	525	990
13	MBEYA	2,616	4,223	6,839
14	MOROGORO	1,337	875	2,212
15	MTWARA	4,035	17,164	21,199
16	MWANZA	1,753	696	2,449
17	NJOMBE	664	1,592	2,256
18	PWANI	781	5,062	5,843
19	RUKWA	145	486	631
20	RUVUMA	1,384	1,825	3,209
21	SHINYANGA	1,704	8,256	9,960
22	SIMIYU	2,443	8,403	10,846
23	SINGIDA	308	412	720
24	SONGWE	183	967	1,150
25	TABORA	2,671	2,032	4,703
26	TANGA	964	941	1,905
JUMLA		**44,572**	**116,707**	**161,279**

SURA YA SITA

6.0 TAARIFA YA UTENDAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA WA KIFEDHA (SACCOS) KWA MIAKA 2024 NA 2025

Vyama vya Ushirika wa Kifedha (Savings and Credit Cooperative Societies – SACCOS) ni sehemu muhimu ya Sekta ya Ushirika nchini Tanzania katika kuwezesha wanachama kupata huduma za kifedha, hususan katika maeneo ya kuweka akiba, kupata mikopo na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi. Uchambuzi katika viashiria vitano vya msingi ambavyo ni

i. Idadi ya SACCOS zilizopewa leseni,
ii. Mtaji wa Msingi,
iii. Jumla ya Mali,
iv. Jumla ya mikopo ambayo bado haijalipwa pamoja na
v. Akiba na Amana.

6.1 HALI YA UTENDAJI WA SACCOS KWA MWAKA 2024 NA 2025

Jedwali Na. 9: Viashiria vya Utendaji wa SACCOS

Kiashiria	Kipimo	2024	2025	Ongezeko	% ya Ukuaji
SACCOS zilizopewa leseni	Idadi	961	981	20	2.08%
Mtaji wa Msingi	Shilingi	201,994,214,917.05	227,809,060,461.61	25,814,845,544.56	12.78%
Jumla ya Mali	Shilingi	1,460,814,811,347.31	1,691,595,179,067.61	230,780,367,720.30	15.80%
Jumla ya Mikopo Ambayo Bado Haijalipwa	Shilingi	1,203,018,070,080.48	1,409,312,753,735.72	206,294,683,655.24	17.15%
Akiba na Amana	Shilingi	1,056,240,180,321.16	1,224,316,722,864.51	168,076,542,543.35	15.91%

6.2 MUHTASARI WA UTENDAJI

Kwa ujumla, utendaji wa SACCOS kwa mwaka 2025 unaonesha mwelekeo chanya wa ukuaji ikilinganishwa na mwaka 2024.

i. Idadi ya SACCOS zilizopewa leseni iliongezeka kutoka 961 mwaka 2024 hadi 981 mwaka 2025, sawa na ongezeko la SACCOS 20 au asilimia 2.08.
ii. Mtaji wa Msingi uliongezeka kwa asilimia 12.78, Mali kwa asilimia 15.80,
iii. Mikopo ambayo bado Haijalipwa kwa asilimia 17.15 na Akiba na Amana kwa asilimia 15.91.
iv. Mikopo Ambayo Bado Haijalipwa ndiyo iliyokuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ukuaji, ikiwa ni asilimia 17.15. Hali hii inaonesha kuongezeka kwa shughuli za

ukopeshaji katika SACCOS na kuongezeka kwa nafasi ya SACCOS katika kutoa huduma za fedha kwa wanachama.

v. Ongezeko la Akiba na Amana la asilimia 15.91 linaonesha kuimarika kwa uwezo wa SACCOS katika kuhamasisha wanachama kuweka akiba na amana.

6.3 UCHAMBUZI WA VIASHIRIA VYA UTENDAJI

SACCOS Zilizopewa Leseni

Idadi ya SACCOS zilizopewa leseni iliongezeka kutoka 961 mwaka 2024 hadi 981 mwaka 2025.

i. Hii ni ongezeko la SACCOS 20, sawa na asilimia 2.08.

ii. Ongezeko hili linaonesha kuendelea kuwepo kwa mahitaji ya huduma za kifedha kupitia mfumo wa ushirika na kuendelea kupanuka kwa wigo wa SACCOS zilizo rasmi na zinazotambulika.

iii. Hata hivyo, ukuaji wa idadi ya SACCOS ulikuwa mdogo ukilinganishwa na ukuaji wa viashiria vya kifedha. Hii inaonesha kuwa sehemu kubwa ya ukuaji wa sekta ilitokana na kuongezeka kwa kiwango cha shughuli za kifedha ndani ya SACCOS zilizopo.

6.4.1 Mtaji wa Msingi

Mtaji wa Msingi uliongezeka kutoka Shilingi 201,994,214,917.05 mwaka 2024 hadi TSh 227,809,060,461.61 mwaka 2025.

i. Hii ni ongezeko la Shilingi 25,814,845,544.56, sawa na asilimia 12.78.

ii. Ongezeko la Mtaji wa Msingi linaonesha kuimarika kwa msingi wa kifedha wa SACCOS. Mtaji wa kutosha ni muhimu katika kuwezesha SACCOS kukabiliana na vihatarishi vya kifedha, kupanua shughuli za ukopeshaji na kuimarisha uendelevu wa taasisi.

iii. Pamoja na ongezeko hilo, kasi ya ukuaji wa Mtaji wa Msingi ilikuwa chini ya ukuaji wa Jumla ya Mali na Mikopo. Hivyo, kuna umuhimu wa kuendelea kuweka mikakati ya kuongeza mtaji sambamba na upanuzi wa shughuli za SACCOS.

6.4.2 Mali

Jumla ya Mali iliongezeka kutoka Shilingi 1,460,814,811,347.31 mwaka 2024 hadi Shilingi 1,691,595,179,067.61 mwaka 2025.

i. Hii ni ongezeko la Shilingi 230,780,367,720.30, sawa na asilimia 15.80.
ii. Ukuaji huu unaonesha kuongezeka kwa ukubwa wa shughuli za SACCOS na kuimarika kwa uwezo wa taasisi katika kumiliki na kusimamia rasilimali za kifedha.
iii. Ongezeko la jumla ya Mali linaashiria mwelekeo mzuri wa ukuaji wa sekta.

6.4.3 Mikopo Ambayo Bado Haijalipwa

Jumla ya mikopo ambayo bado haijalipwa iliongezeka kutoka Shilingi 1,203,018,070,080.48 mwaka 2024 hadi Shilingi 1,409,312,753,735.72 mwaka 2025.

i. Hii ni ongezeko la Shilingi 206,294,683,655.24, sawa na asilimia 17.15. Hiki ndicho kiashiria kilichokuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ukuaji.
ii. Ukuaji huu unaonesha kuongezeka kwa uwezo wa SACCOS kutoa mikopo kwa wanachama. Mikopo hiyo inaweza kuchangia katika kuongeza mitaji ya biashara, kilimo, uwekezaji, ujenzi, elimu na shughuli nyingine za kiuchumi.
iii. Pamoja na kuwa ukuaji wa mikopo ni jambo chanya, unahitaji kuambatana na mifumo madhubuti ya tathmini ya wakopaji, ufuatiliaji wa mikopo, urejeshaji wa madeni na udhibiti wa mikopo chechefu.

6.4.4 Akiba na Amana

Akiba na Amana ziliongezeka kutoka Shilingi 1,056,240,180,321.16 mwaka 2024 hadi Shilingi 1,224,316,722,864.51 mwaka 2025.

i. Hii ni ongezeko la Shilingi 168,076,542,543.35, sawa na asilimia 15.91.
ii. Ukuaji huu unaonesha kuongezeka kwa uwezo wa SACCOS katika kuhamasisha wanachama kuweka akiba na amana.
iii. Akiba na amana ni chanzo muhimu cha rasilimali za kifedha kwa SACCOS na husaidia kuongeza uwezo wa vyama kutoa mikopo kwa wanachama.

6.5 MAFANIKIO MAKUU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2024 HADI 2025

Kwa kuzingatia takwimu, mafanikio makuu ni:

1. Kuongezeka kwa idadi ya SACCOS zilizopewa leseni kutoka 961 hadi 981.
2. Kuongezeka kwa Mtaji wa Msingi kwa asilimia 12.78.
3. Kuongezeka kwa Jumla ya Mali kwa asilimia 15.80.
4. Kuongezeka kwa Mikopo Ambayo Bado Haijalipwa kwa asilimia 17.15.

5. Kuongezeka kwa Akiba na Amana kwa asilimia 15.91.
6. Kuongezeka kwa uwezo wa SACCOS katika kutoa huduma za mikopo.
7. Kuongezeka kwa uwezo wa SACCOS katika kuhamasisha akiba na amana.
8. Kuendelea kukua kwa ukubwa wa sekta ya SACCOS kwa upande wa rasilimali na shughuli za kifedha.

“Sekta ya SACCOS imeendelea kukua mwaka 2025, ikionesha ongezeko katika mtaji, mali, mikopo na akiba na amana. Pamoja na ukuaji huo, kasi kubwa ya ukuaji wa mikopo inahitaji kuambatana na kuimarishwa kwa mtaji, ukwasi na usimamizi wa ubora wa mikopo ili kuhakikisha ukuaji endelevu wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha.”

HITIMISHO

Kwa ujumla, takwimu za Sekta ya Ushirika nchini kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Juni 2026 zinaonesha mwenendo chanya wa ukuaji na mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hadi Juni 2026, jumla ya vyama vya ushirika 6,577 vilikuwa vimesajiliwa kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), vikiwa na wanufaika 3,667,635. Aidha, mauzo ya mazao kupitia vyama yalifikia thamani ya TZS trilioni 4.28, huku ajira 161,279 zikitolewa na vyama vya ushirika. Vilevile, kumekuwa na ongezeko la thamani ya mali za vyama na kuimarika kwa utendaji wa SACCOS katika mtaji, mali, mikopo na akiba na amana.

Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna maeneo yanayohitaji kuimarishwa, ikiwemo uendelevu wa vyama, ushiriki wa wanawake, matumizi ya MUVU, usimamizi wa mali na uwekezaji, pamoja na udhibiti wa mikopo chechefu katika SACCOS. Hivyo, kuna umuhimu wa kuendelea kuimarisha usimamizi, udhibiti, uhamasishaji na utoaji wa huduma za maendeleo kwa vyama vya ushirika, sambamba na matumizi ya mifumo ya kidijitali ili kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi, kamili na kwa wakati.

Taarifa hii ni nyenzo muhimu katika kufuatilia mwenendo wa maendeleo ya Sekta ya Ushirika, kutathmini mafanikio na kubaini changamoto zinazohitaji hatua za maboresho. Matumizi ya takwimu hizi katika kupanga na kufanya maamuzi yatasaidia kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza tija, ushindani na uendelevu wa vyama vya ushirika, kuboresha ustawi wa wanachama na kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa.